Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

TOAM
Tanzania Organic Agriculture Movement

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA
MJUMITA

ANSAF
Agricultural Non State Actors Forum

# UCHAGUZI MKUU NA CHANGAMOTO ZA WAKULIMA WADOGO WADOGO NCHINI

## Je vipi vipaumbele vya wakulima wadogowadogo katika uchaguzi ujao?

Sekta ya kilimo ni sekta inayotegemewa sana katik kukuza uchumi na kuendeleza maisha ya watanzania walio wengi. Hata hivyo sekta hii imeendelea kutawaliwa na wakulima wadogo wadogo ambao ni takribani asilimia 70 ya watanzania wote. Kwa upande mwingine kilimo kinachangia kati ya asilimia 10-14 ya hewa ukaa inayosababisha mabadiliko ya tabianchi na wanaoathirika zaidi na athari za mabadiliko tabianchi ni wakulima wenyewe kwa kuwa wao hutegemea kilimo kwa asilimia 100. Tanzania ina fursa ya kupambana na mabadiliko tabianchi hasa kwa kuboresha njia za kilimo.

MJUMITA kwa kushirikiana na mashirika ya TFCG, TOAM na ANSAF wanatekeleza "Mradi wa Mabadiliko Tabianchi, Kilimo na Kupunguza Umasikini" katika Wilaya ya Kilosa katika vijiji vya Lunenzi, Ibingu, Kisongwe, Chabima na Mfuruni na Wilaya ya Chamwino katika vijiji vya Manchali, Mahama, Nzali Manchali B na Makoja. Lengo la mradi ni kuwajengea uwezo wakulima wadogo wadogo kupunguza umasikini kwa kuboresha mbinu za kilimo ambazo zitawasaidia kukabiliana na athari za mabadiliko tabianchi.

Kwa zaidi ya miaka miwili sasa (toka Oktoba 2012), mradi umekuwa ukitoa mafunzo ya mbinu za kilimo kwa wakulima wadogo wadogo hasa mbinu zinazohifadhi rutuba ya udongo, zinazohifadhi unyevu wa udongo, matumizi bora ya mbolea za asili, matumizi ya mbegu za asili zilizoboreshwa ambazo zinakomaa kwa muda mfupi na ambazo zinastahimili ukame, lakini pia namna ambavyo wanaweza kuyafikia masoko ya mazao wanayozalisha.

Mbinu hizi zimesaidia kuleta tija kubwa kwa wananchi wengi ambao wamezijaribu ikiwa ni pamoja na kuongeza faida kwa wakulima. Mfano, wakulima ambao waliweza kuzitekeleza vizuri waliongeza uzalishaji kutoka wastani wa magunia 5 kwa ekari mpaka kufikia wastani wa magunia 15.

Hata hivyo pamoja na mafanikio makubwa ya mbinu hizi mpya za kilimo kwa wakulima wadogo wadogo katika kupunguza umasikini na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kumekuwa na changamoto kadhaa zinazowakwamisha wakulima kunufaika zaidi. Kwa kuwa nyingi ya changamoto za wakulima zinaweza kutafutiwa ufumbuzi kwa urahisi na utashi wa Serikali na viongozi wa kuchaguliwa, wakulima kutoka vijiji vya Kisongwe, Ibingu, Lunenzi, Chabima, Mfuruni, Ludewa na Mvumi Wilayani Kilosa, walikutana mapema mwezi wa 6 ili kutafakari kwa kina changamoto wanazokabiliana nazo ili wakati wa kampeni wasisitize wagombea kufahamu changamoto zao. Katika mkutano huo ambao uliuhudhuriwa na wataalamu wa wilaya, waheshimiwa madiwani na wakulima walitoa mapendekezo ya namna ambavyo kila changamoto waliyoiibua inaweza kushughulikiwa. Changamoto hizi ni kama ifuatavyo:

- **Miundo mbinu mibovu ya barabara na mawasiliano;** Wakulima walio wengi wanaishi vijiji ambavyo bado havifikiki kirahisi kwa misimu yote ya mwaka na hivyo kushindwa kupeleka mazao yao kwenye masoko ya uhakika. Matokeo yake wakulima wadogo wadogo wamekuwa wakiuza mazao yao kwa walanguzi wanaotembelea vijiji vyao kwa bei ya hasara na maisha yao kuendelea kuwa duni kila siku. Aidha vijiji vingi bado havina mawasiliano ya simu na hivyo wakulima kukosa fursa ya kufahamu bei ya soko la mazao yao kabla ya kuyauza kwa walanguzi na hivyo walanguzi kutumia fursa hiyo kuwalangua wakulima.
- **Kucheleweshwa kwa pembejeo za kilimo;** Ili wakulima waweze kuzalisha zaidi na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ni muhimu sana kuwa na pembejeo bora za kutosha na kwa wakati. Asilimia kubwa ya pembejeo za kilimo ambazo hutolewa na Serikali huwafikia wakulima zikiwa zimechelewa na hivyo kutokuwa na msaada wowote kwa wakulima.
- **Viongozi kutosimamia sheria na miongozo ya kilimo na mazingira;** Kumekuwa na mapungufu makubwa katika usimamiaji wa sheria ndogo ndogo za kilimo na misitu na kupelekea kilimo kufanyika katika maeneo yasiyotengwa na kusababisha uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na misitu na uharibifu wa vyanzo vya maji. Uharibifu wa misitu hasa unaotokana na kilimo


*Mkulima Bw. Ally kutoka kijiji cha Ibingu akipima nyanya kwenye ndoo ambazo zinawakandamiza wakulima.*




*Mkulima Bw.Kipara kutoka kijiji cha Ibingu amenunua pikipiki baada ya kulima nyanya kwa kutumia mbinu za kilimo rafiki na mazingira na anaitumia kupeleka mazao yake sokoni.*



*Maharage yaliyopatikana kutokana na kilimo rafiki na mazingira*





*Mkulima Bi Susan kutoka kijiji cha Kisongwe ambaye hayupo ndani ya mradi akichuma mboga ambazo amezipanda kwa kutumia mbinu za kilimo rafiki na mazingira.*



*Shamba la mtama katika kijiji cha Nzali Wilayani Chamwino*

cha kuhama hama kimekuwa kikichangia athari za mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima wadogo wadogo.

- **Wakulima kukosa fursa ya kukopeshwa na taasisi za kifedha;** Wakulima wadogo wadogo wanakosa fursa ya kupata mikopo toka taasisi mbalimbali za kifedha ili kuwekeza kwenye kilimo na hii inasababishwa na kutokurasimishwa kwa ardhi zao na kupatiwa hati miliki.

- **Maeneo makubwa ya ardhi kumilikiwa na wawekezaji wachache;** Maeneo mengi ya ardhi yanamilikiwa na wawekezaji wachache wakiwaacha wakulima wadogo wadogo wakiwa hawana maeneo ya kilimo ya kutosha. Ugawaji huo wa ardhi umekuwa ukifanyika bila kuwashirikisha wananchi wa maeneo husika na kupelekea migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima wadogo wadogo na wawekezaji.

- **Ongezeko la migogoro ya wakulima na wafugaji:** Kumekuwepo na migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji inayotokana na aidha kutokuwepo kwa mipango ya matumizi bora ya ardhi au kutosimamiwa vizuri kwa mipango bora ya ardhi na hivyo kupelekea vifo na ulemavu kwa baadhi ya wananchi. Migororo hii ya ardhi imekuwa ikizorotesha juhudi za wakulima katika kuongeza uzalishaji na kupambana na umasikini

## Mapendekezo ya wakulima wadogo wadogo kwa wananchi wanaogombea nafasi mbali mbali za uongozi katika uchaguzi mkuu.

- Serikali itakayoingia madarakani itoe kipaumbele katika kuendeleza huduma za jamii vijijini kama barabara, zahanati, shule, masoko na mitandao ya simu. Vile vile kiongozi atakayechaguliwa ahamasishe wananchi kuanzisha vituo vya kuuzia mazao na kusimamia sheria ndogo za kuzuia wafanyabiashara wasio waaminifu kutumia vipimo visivyo sahihi vinavyowaibia wakulima mazao yao na Serikali kutopata kodi stahiki.

- Viongozi watakaoingia madarakani wahakikishe kwamba bajeti kwa ajili ya kilimo inaongezwa ili kufikia maazimio ya mkutano wa Maputo (asilimia 10 ya bajeti ya Serikali ielekezwe kwenye sekta ya kilimo. Hii itaboresha upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati, utoaji wa elimu ya ugani kwa wakulima na utatuzi wa changamoto za masoko.

- Viongozi watakao chaguliwa waweke mkazo katika kuwajibisha watendaji ambao watashindwa kusimamia mipango na sheria ndogo za usimamizi wa misitu na kilimo. Pia elimu ya kilimo na mazingira iendelee kutolewa kwa wadau mbalimbali ili kila mtu afahamu wajibu wake na kuutekeleza.

- Viongozi watakao chaguliwa watoe kipaumbele katika kutengeneza na kuisimamia kikamilifu mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji, kupima ardhi na wananchi wamilikishwe ardhi zao kisheria. Hii itasaidia wakulima kuwa na hadhi ya kukopesheka na hivyo kuendeleza shughuli zao za kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi.

- Viongozi watakao chaguliwa wahakikishe kuwa michakato ya ugawaji na umilikishaji wa maeneo ya ardhi kwa wawekezaji inafuata taratibu za nchi, inafanyika kwa uwazi na wananchi wanashirikishwa kikamilifu ili kuepuka migogoro mikubwa kati ya wakulima na wawekezaji, kutokana na wananchi kukosa maeneo ya kutosha kwa ajili ya kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi..

- Ili kuepusha migogoro ya wakulima na wafugaji, Serikali itakayochaguliwa iwekeze katika kuboresha maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za ufugaji ili wafugaji wabaki katika maeneo yao. Hii ni pamoja na kuweka miundombinu ya maji na malisho kwenye maeneo ya ufugaji.



*Wanachi wakiwa pamoja na diwani wa kata ya Lumuma (Mwenye Miwani) wakijadili mambo ambayo wangependa yawekwe kwenye ilani za vyama.*



*Mkulima Bw. Kiliani kutoka kijiji cha Kisongwe akiwaelekeza wanafunzi wa shule ya msingi Lumuma namna ya kutumia mbinu za kilimo rafiki na mazingira na namna zinavyoleta tija.*

Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) chini ya "Mradi wa Mabadiliko ya Tabia nchi, Kilimo na Kupunguza umasikini"

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

**MJUMITA**

Mtandao wa jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA)
S.L.P 21522, Dar es salaam | Simu: +255 22 2669007
Barua pepe: mjumita.org@mjumita.org | Tovuti: www.mjumita.org